# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA SITA

**05 NOVEMBA, 2024**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA SABA

## KIKAO CHA SITA – TAREHE 05 NOVEMBA, 2024

**I. DUA:**

**II. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**88. MHESHIMIWA TUNZA ISSA MALAPO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Halmashauri ya Mtwara Mikindani ilikusanya kiasi gani cha Ushuru wa Magari yanayosafirisha Makaa ya Mawe kwa Mwaka 2022/2023.

**89. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itajenga OPD na Wodi za Wagonjwa katika Kituo cha Afya Kintinku.

**90. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Maboma mangapi ya Zahanati hayajakamilika Wilayani Kyerwa na lini yatakamilika.

**91. MHESHIMIWA TABASAM HAMIS MWAGAO (SENGEREMA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatekeleza ahadi ya Ujenzi wa km 15 wa barabara za Sengerema Mjini kwa kiwango cha lami.

**92. MHESHIMIWA DOROTHY GEORGE KILAVE (TEMEKE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kuna mpango gani wa kujenga kwa Zege barabara zinazoingia Bandari Kavu - Temeke.

## WIZARA YA NISHATI:

**93. MHESHIMIWA YAHYA ALLY MHATA (NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali italipa fidia kwa Wananchi wa Wilaya ya Nanyumbu ili kupisha ujenzi wa Gridi ya Taifa.

**94. MHESHIMIWA DKT. JASSON SAMSON RWEIKIZA (BUKOBA VIJIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itapeleka Umeme Vitongoji visivyokuwa na umeme Bukoba Vijijini.

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

**95. MHESHIMIWA FATMA HASSAN TOUFIQ (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Wanafunzi wangapi wamerudi shuleni baada ya kujifungua, tangu Serikali iruhusu Wanafunzi hao kuendelea na masomo.

96. **MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa Elimu ya Uzalendo kwa Wananchi wakati Taifa lipo katika mageuzi makubwa ya uchumi.

**WIZARA YA KILIMO:**

97. **MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, kuna mkakati gani wa kupandisha kiwango cha mauzo ya Kahawa kitakacholipwa Benki badala ya shilingi milioni moja inayolipwa kwa sasa.

**WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

98. **MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo:-

Je, upi mkakati wa kuongeza thamani ya zawadi kutoka Shilingi Laki Moja na Elfu Hamsini hadi Milioni Kumi kwenye Tamasha la Utamaduni Nchini.

**WIZARA YA FEDHA:**

**99. MHESHIMIWA JACQUELINE NGONYANI MSONGOZI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza kodi ya uingizaji wa vyakula vya samaki nchini.

**WIZARA YA AFYA:**

**100. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, nini chanzo cha ongezeko la Wagonjwa wa Figo nchini.

**WIZARA YA MAJI:**

**101. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Vitongoji vya Kimele, Kilemela na Nyakahamba katika Kata za Mapinga na Kerege vitapata maji ya uhakika.

**102. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria wa Rorya - Tarime utakamilika kwa kuwa kasi ya utekelezaji ni ndogo sana.

**WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**103. MHESHIMIWA NOAH LEMBURIS SAPUTU (ARUMERU MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Minara itajengwa Vijiji vya Kata ya Bwawani, na Vijiji vya Nengung'u, Oloitushula, Olchorovus, Engutukoit, Losinoni Juu na Losinoni Kati.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**104. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Muswada wa Sheria ya Sekta Binafsi ya Ulinzi utaletwa Bungeni kwa kuwa Kampuni Binafsi za Ulinzi zilianzishwa bila Sheria wala Kanuni.

**105. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA (KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, lini Serikali itajenga Kituo cha Polisi katika Jimbo la Kilindi.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**106. MHESHIMIWA SAASHISHA ELINIKYO MAFUWE (HAI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani wa kuanza kutoa Ruzuku Vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro kutoka kwenye mapato ya Mlima.

## III. KAMATI YA MIPANGO:

### WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### WAZIRI WA FEDHA:

Kwamba, Bunge lipokee, kujadili na kushauri kuhusu Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA**
**05 NOVEMBA, 2024**

**BARAKA I. LEONARD**
**KATIBU WA BUNGE**